*Namba ya Mtahiniwa*____________________________

*Jina la Shule* __________________________________

*Mkoa*_________________________________________

*Wilaya*________________________________________

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**SAMPULI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI**

**01** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 1:40** **Mwaka: 2024**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **sita (6)**.
2. Jibu maswali **yote** kwenye nafasi ulizopewa.
3. Sehemu A na B zina alama **ishirini (20)** kila moja na sehemu C ina alama **kumi (10)**.
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**, **isipokuwa** katika michoro ambapo ni lazima kutumia penseli.
5. Vifaa vya mawasiliano visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** na taarifa zote muhimu katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

| **KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU** | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAHIHI YA MTAHINI** |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAHIHI YA MHAKIKI** | | |

***Namba ya Mtahiniwa*____________________________**

***Jina la Shule*__________________________________**

***Mkoa*__________________________________________**

***Wilaya*_________________________________________**

## SEHEMU A (Alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Sikiliza kwa makini hadithi utakayosomewa na msimamizi, kisha jibu kipengele cha (i) – (v), **kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi** na kuandika katika kisanduku.

(i) Kwa nini mfalme alikuwa anavaa kilemba kinachofunika kichwa na masikio?

A Alikuwa na masikio kama ya punda.
B Alikuwa na nywele ndefu zenye mvi.
C Alikuwa na kichwa kama cha punda.
D Alikuwa na kipara kama ngoma.
E Alikuwa na kichwa kidogo kama mpira.

(ii) Kinyozi aliyemnyoa mfalme alikuwa anaitwa nani?

A Nguvumali B Askari C Punda
D Roporopo E Hekaheka

(iii) Mfalme alimwambia nini kinyozi kabla ya kuanza kumnyoa?

A Asicheke wala kusema atakachoona.
B Acheke ila asiseme atakachoona.
C Atangaze atakachoona.
D Atakachoona aseme kwa watu.
E Atakachoona asisema popote.

(iv) Kipi kilisababisha siri ya mfalme Nguvumali kufahamika kijijini?

A Sauti kutoka katika mti B Mfalme mwenyewe alitoa siri
C Wanakijiji wa hekaheka D Upepo mkali
E Dunia kutokuwa na siri

(v) Mfalme alifanya nini baada ya wanakijiji kujua kuwa ana masikio kama ya punda?

A Aliwaadhibu askari wake B Alimfunga kinyozi wake
C Aliamua kuvua kilemba D Alimuua kinyozi wake
E Alisikitika sana

***Namba ya Mtahiniwa*____________________________________**

***Jina la Shule*  ____________________________________**

***Mkoa*____________________________________________**

***Wilaya*__________________________________________**

2. Katika kipengele cha (i) - (x), **chagua jibu sahihi** kisha andika herufi yake katika kisanduku ulichopewa.

(i) Kitendawili kipi kati ya vifuatavyo kinateguliwa na picha ifuatayo?



A Ana miguu kama msumeno.
B Hujihami bila silaha.
C Ana mdomo lakini anauma kwa mkia.
D Mama hana miguu lakini mtoto anayo.
E Rafiki yangu mpole lakini adui wanamhara.

(ii) "Wanakijiji wa Kilolo hufanya kazi kwa kushirikiana." Ni methali ipi kati ya zifuatazo inaweza kutumika kuwashauri wanakijiji hao kuendelea na ushirikiano?

A Dhahabu hupewa aliyeshinda.
B Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.
C Damu nzito kuliko maji.
D Lakuvunda halina ubani.
E Haraka haraka haina Baraka.

***Namba ya Mtahiniwa*** ____________________________

***Jina la Shule*** ____________________________

***Mkoa*** ____________________________

***Wilaya*** ____________________________

(iii) Kitendawili kipi kati ya vifuatavyo kinateguliwa na kiumbe aliyeko kwenye picha ifuatayo?



A Kila niendapo hunifuata.
B Anajenga ingawa hana mikono.
C Hana adabu wala staha kwa watu.
D Bibi yangu hutembea na nyumba yake.
E Daima hunifuata nyuma, nikimfuata hukimbia.

(iv) "Mwanafunzi amechelewa darasani." Sentensi ipi inakanusha sentensi hiyo?
A Mwanafunzi hatachelewa darasani.
B Mwanafunzi hajachelewa darasani.
C Mwanafunzi hachelewi darasani.
D Mwanafunzi huwa hachelewi darasani.
E Mwanafunzi hakuchelewa darasani.

(v) "Wao wanapenda kucheza mpira". Sentensi hiyo inaonesha nafsi gani kati ya zifuatazo?
A Nafsi ya tatu wingi  B Nafsi ya pili umoja  C Nafsi ya pili wingi
D Nafsi ya tatu umoja  E Nafsi ya kwanza wingi

***Namba ya Mtahiniwa*****____________________________**

***Jina la Shule*** **___________________________________**

***Mkoa*****__________________________________________**

***Wilaya*****_________________________________________**

(vi) Soma mazungumzo yafuatayo kisha jibu swali linalofuata:
**Tumbo**: *Kadiri unavyoendelea kuishi hapa ninaanza kukuchoka.*
**Legelege**: *Ninaona hutaki kusema kwa uwazi. Unataka niondoke?*

Methali ipi kati ya zifuatazo inahusiana na kauli iliyotolewa na Legelege?

A Umdhaniaye ndiye kumbe siye.
B Akufukuzaye hakwambii toka.
C Mtaka yote kwa pupa hukosa yote.
D Chanda chema huvikwa pete.
E Akupigaye shavu moja mgeuzie la pili.

(vii) "Watoto watukutu hufitiniana." Kauli gani ya matendo inayojidhihirisha katika sentensi hiyo?

A Kutendwa    C Kutendea    E Kutendeka
B Kutendeana    D Kutenda

(viii) Mwalimu alituambia, "Ingieni darasani." Kauli taarifa ya sentensi hii ni ipi kati ya zifuatazo?

A Mwalimu aliwaambia tuingie darasani.
B Mwalimu alisema mmeingia darasani.
C Alituambia mwalimu tuingie darasani.
D Mwalimu alituambia kuwa tuingie darasani.
E Mwalimu aliwaambia kuwa waingie darasani.

***Namba ya Mtahiniwa***____________________________

***Jina la Shule*** ___________________________________

***Mkoa***_________________________________________

***Wilaya***________________________________________

(ix) Chunguza jedwali lifuatalo, kisha uchague neno la Kiswahli linalopatikana katika jedwali hilo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| V | Z | W | G | U |
| P | R | D | H | F |
| K | U | K | U | J |
| B | S | V | T | N |
| H | G | I | Z | M |

A Bata B Kuku C Meza D Kiti E Giza

(x) Sokomoko alitaka kununua samaki lakini alisahau kutembea na pesa. Kauli ipi inaeleza hali hiyo?

A Sokomoko angesahau pesa angenunua samaki.
B Sokomoko asingesahau pesa angenunua samaki.
C Sokomoko angelisahau pesa asingelinunua samaki.
D Sokomoko asingelisahau pesa asingelinunua samaki.
E Sokomoko angelisahau pesa angelinunua samaki.

3. Oanisha maana ya aina za maneno zilizopo **Orodha A** na aina za maneno kutoka **Orodha B**, kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika nafasi ya majibu.

| Orodha A | | Majibu | Orodha B |
|---|---|---|---|
| (i) | Hutoa taarifa zaidi kuhusu kitenzi na kivumishi. | ( ) | A. Kihusishi |
| (ii) | Husimama peke yake na kutoa taarifa iliyokamilika. | ( ) | B. Kiunganishi |
| (iii) | Hufanya kazi ya kuhusisha maneno katika tungo au sentensi. | ( ) | C. Nomino<br>D. Kihisishi |
| (iv) | Hutoa taarifa za nyongeza kuhusu nomino au kiwakilishi. | ( ) | E. Kielezi<br>F. Kitenzi<br>G. Kivumishi |
| (v) | Huonesha hisia za watu kama vile mshangao, huzuni, huruma, hasira na furaha. | ( ) | |

***Namba ya Mtahiniwa*___________________________**

***Jina la Shule*** ___________________________________

***Mkoa***__________________________________________

***Wilaya***_________________________________________

**SEHEMU B (Alama 20)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

4. Taja visawe vya maneno yafuatayo kwa kuandika jibu katika nafasi iliyoachwa wazi.
   (i) Pasua ____________________________________________________________
   (ii) Idhini____________________________________________________________
   (iii) Mtoto____________________________________________________________
   (iv) Bibi____________________________________________________________
   (v) Kanuni____________________________________________________________

5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali katika kipengele cha (i) - (v) **kwa kuandika jibu sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

Binti yangu nisikie, dunia hii dunia,
Wengi wasikitikie, imewaua tamaa,
Mali sipapatikie, utakufa kwa tamaa,
Yakikukuta madhara, majuto ni mjukuu.

Kataa vijizawadi, kutoka kwa vijibaba,
Kujichunga huna budi, kuepuka ukahaba,
Mwili usije unadi, maradhi yakakukaba,
Yakikukuta madhara, majuto ni mjukuu.

Nawe njemba wa kiume, sione dunia tamu,
Maradhi hayana shime, ukipenda vya haramu,
Bangi nayo usiseme, imeshashika hatamu,
Yakikuta madhara, majuto ni mjukuu.

Tatiwa korokoroni, ulofa kiendekeza,
Serikali i makini, maovu kutokomeza,
Taishia gerezani, tamaa ikikumeza,
Yakikukuta madhara, majuto ni mjukuu.

***Namba ya Mtahiniwa***_________________________

***Jina la Shule*** _______________________________

***Mkoa***_____________________________________

***Wilaya***____________________________________

Wino unaishilia, hayo yatie moyoni,
Jina langu Vumilia, mzee wa msituni,
Vijana nawalilia, msijisweke motoni,
Yakikukuta madhara, majuto ni mjukuu.

**Maswali**

(i) Katika shairi ulilosoma, mshairi anasisitiza jambo gani kwa binti yake?

______________________________________________________

______________________________________________________

______________________________________________________

(ii) Binti anaweza kupata madhara gani endapo ataendekeza tabia zilizotajwa kwenye ubeti wa pili?

______________________________________________________

______________________________________________________

______________________________________________________

(iii) Mshairi anampa kijana wa kiume tahadhari gani katika ubeti wa tatu?

______________________________________________________

______________________________________________________

______________________________________________________

(iv) Mshairi anamaanisha nini anaposema “msijisweke motoni?”

______________________________________________________

______________________________________________________

______________________________________________________

***Namba ya Mtahiniwa*** ____________________________

***Jina la Shule*** ___________________________________

***Mkoa*** __________________________________________

***Wilaya*** _________________________________________

(v) Mshairi anatoa ujumbe gani katika shairi ulilosoma?

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

**SEHEMU C (Alama 10)**

Jibu Swali la **Sita (6)**.

6. Mwandikie Mwalimu Janeth Matesha kadi ya mwaliko wa kuhudhuria tafrija ya kumpongeza dada yako Eliza aliyehitimu masomo ya chuo kikuu. Familia yenu ni ya Bwana na Bibi John Samweli. Tafrija hiyo itafanyika tarehe **22/11/2024** kwenye Bwalo la Polisi, Lushoto, kuanzia saa **7:00** mchana hadi saa **12:00** jioni.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# SAMPULI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

**01** **KISWAHILI**

## MAELEKEZO KWA MSIMAMIZI

Zingatia yafuatayo **kabla ya kusoma maelekezo** kwa watahiniwa:

(i) Hakikisha unasoma hadithi kwa **sauti** na **taratibu** kwa mara ya kwanza huku ukizingatia alama zote za uandishi zilizopo katika hadithi hiyo. Unaposoma kwa mara ya pili ongeza kidogo kasi ya usomaji.

(ii) Muda utakaotumika kuwasomea watahiniwa hadithi ni **dakika tano** (**05**) na muda utakaotumika kwa watahiniwa kujibu maswali ni **dakika tano** (**05**). Sehemu hii itafanyika kwa **dakika kumi** (**10**).

(iii) Wakati utakapokuwa unasoma hadithi, hakikisha kuwa watahiniwa hawafungui karatasi yenye maswali ya mtihani.

(iv) Soma kwa sauti maelekezo kwa watahiniwa (1 hadi 4).

## MAELEKEZO KWA WATAHINIWA

1. Nitasoma **kwa sauti** hadithi mara mbili, hivyo kila mmoja asikilize kwa makini.
2. Nitakapokuwa nasoma hadithi hakikisha kuwa karatasi yako ya maswali haijafunguliwa.
3. Nikisoma hadithi kwa mara ya kwanza, sikiliza bila kujibu maswali na nikimaliza kusoma kwa mara ya pili, jibu swali la 1 (i) hadi (v) kisha endelea kujibu maswali mengine (2 hadi 6).
4. Naanza kusoma hadithi sasa hivyo **sikiliza kwa umakini**.

# SIRI

## HADITHI

Hapo zamani za kale palikuwa na Mfalme aliyeitwa Nguvumali katika nchi ya Hekaheka. Mfalme aliwapenda sana raia. Hata hivyo, Mfalme huyo alikuwa hana raha kwa kuwa alikuwa na siri moyoni. Ukweli ni kwamba, Mfalme alikuwa na masikio kama ya Punda. Hali hii ilimfanya avae kilemba kila siku kinachofunika kichwa na masikio.

Siku moja Mfalme alimuita Roporopo ili amnyoe nywele. Roporopo alipofika alikaribishwa na askari na kuingia katika chumba cha mfalme. Kabla ya kuanza kumnyoa mfalme, aliambiwa na mfalme kuwa atakachoona asiseme popote. Baada ya kumaliza kumnyoa, Roporopo aliondoka na kwenda porini. Alipofika huko alichimba shimo refu kisha akaingia mle na kusema kwa sauti, “Mfalme Nguvumali ana masikio kama ya Punda.” Baadaye mti uliota kwenye lile shimo na kurefuka.

Upepo mkali ulipovuma miti ilitikisika. Ndipo ule mti ulitoa maneno kwa sauti kuelekea kijijini, yalisikika maneno yakisema, “Mfalme Nguvumali ana masikio kama ya Punda.” Mfalme aliposikia yale maneno alisema, “Ama kweli dunia haina siri.” Mwishowe, Mfalme aliamua kuvua kilemba na kukubali watu wajue kuwa ana masikio kama ya Punda.